MASUALI KWA MUHADDITH WA AL-MADÎNAH, AL-‘ALLÂMAH ‘ABDULMUHSIN AL-‘ABBÂD AL-BADR KUHUSIANA NA DA’WAH YA SALAFY NCHINI SYRIA

MAJIBU YA MASUALI[1]

Bismillāh, ir-Rahmān ir-Raheem

Suali la kwanza: “Sheikh wetu, sisi tuna ta’sisi katika nchi ya Syria, kwa jina la “Markaz Imām al-Albānī li’d-Da’wah wa’l-Irshād”, na ipo katika mitihani ya kudhoofika kwa upande wa ukosefu wa usaidizi wa ki-Da’wah, ingawa inapata usaidizi mzuri wa vifaa tena wenye kutegemeka kutoka kwa baadhi ya matajiri kutoka kwenye miradi mengi inayotokamana na baadhi ya ndugu zetu wazuri. Juhudi zetu za ki-Da’wah zimelenga kwenye madarasa ya watoto, makongamano ya ki-ilimu kwa watu wazima, uchapishaji na usambazaji wa vitabu vya wanavyuoni, kama vile Sheikh al-Albâni, Ibn Bâz, Ibn ‘Uthaymîn na Fawzân. Katika mazingira haya, ndugu kutoka kwenye “Jam’iyyat Ihyā ut-Turāth” wamejitolea kutusaidia katika njia hii ya Da’wah khususan na Ta’sisi yetu yote kwa ujumla, bila ya kutuwekea masharuti yoyote mbali na kuwa na mipangilio na usajili wa kisheriya. Wamesema: “Ndugu kutoka “Jam’iyyat Ihyā ut-Turāth al-Islāmī” wamekiri yakwamba sisi tuna makosa, lakini licha ya hayo tunataka kushirikiana na ma-Salafi. Kutokana na shughuli hizi na ndugu hawa, baadhi ya ndugu wengine walitulaumu sisi na baadhi yao wakatuorodhesha sisi na kundi na kuanza kuwatahadharisha watu dhidi yetu. Ni nini rai yako kuhusiana na jambo hili?

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-‘Allâmah ‘AbdulMuhsin al-Abbâd:

Hao wanaowalaumu nyinyi na waje na mbinu mbadala, ni mbinu gani walizowaletea wao badala ya hilo wanalowakataza musifanye? Hawa ndugu zetu kutoka Jam’iyyat Ihyā ut-Turāth wana juhudi nzuri sana, wao wanawasambazia wanafunzi wa ki-ilimu, kiwango kikubwa sana cha vitabu ulimwengu mzima, na wanafanya juhudi za hisani za kuwasaidia Waislamu. Hapana shida kushirikiana nao, hata ingawa wana makosa.

Suali la pili: “Sheikh wetu, imesambazwa kwenye mitandao na kwenye makundi ya WhatsApp, pakiwemo ndugu fulani ma-Salafi wenye asili ya ki-Syria ambao wanaotahadharisha watu na kuwafanyia tabdî’ baadhi ya Mashekhe, na wanafunzi wakubwa wa ki-‘ilmu kama vile: Sheikh ‘Abdul’Azeez ar-Rayyis, ‘Abdullāh al-’Ubaylān, Mashhūr bin Hasan Āl Salmān, ‘Ali al-Halabī, Ibrāheem ar-Ruhaylī, ‘Abdul’Adheem Badawī, Sālim at-Taweel, ‘AbdulMalik ar-Ramadānī. Jambo hili limesababisha vijana kuanza kupeana majina na kukatana (kususiana), hata ingawaje ma-Salafi wa Syria ni

wachache mno, haliyakuwa wapinzani wao kutoka katika pote la ma-Sufi, Takfiri na ma-Hizbi ni wengi. Wote hao wanafanya njama dhidi yetu, na kwa hakika hali yetu haikufichika kwako."

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-Abbâd:

Usishangazwe na matukio haya yenye kusambaa kwenye miji ya Syria, kwani yamesambaa mpaka sehemu za Uropa, mahali ambapo idadi ya Waislamu ni chache mno. Usiyaangalie mas'ala haya na musijishughulishe nafsi zenu na watu hao, na jitahadharini nao haswa, jishughulisheni na kutafuta 'ilmu na kuwafundisha watu. Sasa lau kama sisi tutakapotahadharishwa na hao [Mashekhe waliotajwa], atabakia nani?

Suali: "Ewe Sheikh wetu, ni kina nani Ma'ulamaa wa zama zetu hizi?"

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-Abbâd:

Ma'ulamaa tuliowahi kuwaona baada ya mwaka wa 1400 AH walikuwa ni Al-Albâni, Ibn Bâz na Ibn 'Uthaymîn, ama sisi wengine basi ni wanafunzi wa ki-'ilmu.

Suali: "Walio miongoni mwa ambao wangali hai?"

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-Abbâd:

Kamuulize Sheikh Sālih Fawzān.

Suali: "Ni zipi tafsiri nzuri kwa wasomi chipukizi?"

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-Abbâd:

Tafsiri ya as-Sa'dî, hiyo ndiyo tafsiri ya pekee inayoweza kusomwa na watu wa kawaida.

Suali: "Ewe Sheikh wetu, unatunaswihi nini kuhusiana na Usūl ul-Fiqh?"

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-Abbâd:

Mudhakkirat Usūl ul-Fiqh cha Shaykh al-Ameen ash-Shanqītī.

Suali: "Sheikh wetu, na kuhusu fiqhi?"

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-'Allâmah 'AbdulMuhsin al-Abbâd:

Fatāwā za Shaykh ul-Islām [Ibn Taymiyyah] na *Fatāwā* za Shaykh Bin Bāz *(rahimahumullāh)*.

Suali: "Sheikh wetu, watu wengi wa kawaida na baadhi ya wanafunzi wa ki-'ilmu, humsikiliza Abū Ishāq al-Huwaynī, na baadhi yao wameujuwa Usalafiyyah kitambo kwa kupitia kwenye kanda za tepu za Sheikh [Abū Ishāq], na baadhi ya watu bado wanamfuata yeye kwenye setilaiti, na ana darasa za mawaidha na ta'luma za masomo

ya hadîth. Baadhi ya wanavyuoni wanamzungumza yeye, sasa jee, tutahadharishe watu dhidi yake?.”

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-‘Allâmah ‘AbdulMuhsin al-Abbâd:

Laa! Musiwatahadharishe watu dhidi yake na mimi sijui kuhusu jambo lolote linalomstahiki alaumiwe kwalo. Lau kama sisi tutawatahadharisha watu dhidi yake, basi nnani atakaebaki? Awapo ana makosa yoyote, sisi tuwatahadharishe watu kuyahusu hayo makosa.

Suali: “Sheikh, hii ina maana yakwamba anaweza kusikilizwa na watu wafaidike kutoka kwake?

Jawabu kutoka kwa Muhaddith wa Madînah, al-‘Allâmah ‘AbdulMuhsin al-Abbâd:

“Na’am, msikilizeni na mufaidike kutoka kwake.”

[1] Kutokamana na masuali aliyoulizwa Muhaddith wa Madînah na baadhi ya ndugu kutoka Syria na yakaulizwa na ndugu ‘Ameed Zarzūr mnamo 17th Dhu’l-Hijjah 1435 AH/11th October 2014, ba’dal ‘Asr. Muhaddith wa Madînah, al-‘Allāmah ‘AbdulMuhsin aliwaruhusu waandike majibu yake na wala wasisajili sauti:

http://d.pr/f/xbhh

Imefasiriwa na Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad;

THE QUR’AN AND SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA.

MOMBASA.

www.qssea.net

QSSEA